

UBATIZO WA MAJI

==========

kulingana na Biblia na Marejeo ya Kihistoria yanayoendana na Mafundisho na Utendaji wa Kanisa la Kwanza, 33-100 B.K.

UAMSHO WA JINA



Kimetungwa na Lewis Manuwal
Mtafsiri Rev. Goodluck Massawe-Tanzania

Unatakiwa wewe Uzamishwe au Unyunyiziwe wakati Unapobatizwa?

Ujumbe wa mwisho aliouhubiri Yesu ulikuwa ni agizo Kubatiza mataifa yote (Mathayo 28:19)

Ujumbe wa kwanza waliouhubiri Mitume ni matokeo ya agizo la kila mmoja kubatizwa. (Matendo 2:38)

Ubatizo ni wa muhimu na unatakiwa ufanyike kulingana na Maandiko.

Hapa chini ni mpango wa safu mbili zinazoonyesha maandiko ya kuzamisha na kunyunyizia.

Kuzamisha	***Kunyunyizia***

Maji mengi
"Yohana alikuwa akibatiza huko Ainoni kwa sababu kulikuwa na maji tele"
(Yohana 3:23)

Ndani ya Maji
"Wote wawili wakateremka majini."
(Matendo 8:39)

Kuzikwa katika Maji
"Wakapanda kutoka majini"
(Matendo 8:39)

Kuzikwa ndani ya Maji
"Tumezikwa pamoja naye kwa njia ya Ubatizo" (Warumi 6:4)

Kuoteshwa ndani ya Maji
"Kuunganika pamoja naye"
(Warumi 6:5)

Bila mashaka Kanisa la kwanza lilifundisha na kutenda ubatizo kwa kuzamisha. Paulo alisema, "Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi Injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri na alaaniwe" (Wagalatia 1:8-9)

Endapo utaratibu wa ubatizo wako hauwezi kupatikana ndani ya Biblia! Je! huogopi kuutenda?

-1-

KUZAMISHA AU KUNYUNYIZIA?

Hapa chini ni orodha ya maandishi ya wanauzuoni na waandishi wasomi wa Biblia, na mamlaka katika somo hili. Marejeo mengi katika haya yanaweza kupatikana katika maktaba katika eneo lako.

---- 'Baptizo'----

Greek-English Lexicon kilichotolewa na Liddel Scott & Thayer	**Ubatizo ni neno lililochukuliwa kutoka Kigiriki lenye maana Kutumbukiza, kuzamisha**
Clasic Greek-English Kamusi ya Pollet	**Neno la Kigirki Baptizo linamaanisha kuzamisha**
Kamusi ya Kigiriki kwa Kiingereza Iliyotolewa na Divry's	**Neno Baptizo ni kuzamisha**
Emphatiki-Dioglot inayo maneno ya asili maandishi ya Kigiriki.	**Katika tukio lolote neno la Baptizo lilimaanisha kuzamisha.**

----MAMLAKA----

Encyclopedia ya Kidini ya Scaff-Herzog	**Mara zote ubatizo ulikuwa ni maziko. Agizo la kubatiza lilikuwa ni kuzamisha. Toleo 1, Ukurasa 451**
Encyclopedia ya Biblia ya Kikatoliki	**Kuzamisha ndiyo njia ya kale iliyotumika. Warumi 6:4 Ukurasa 61, Aya ya 2**
Encyclopedia Dictionary of the Bible	**Ni wazi kwamba tendo la ubatizo lililotendeka kwenye ubatizo ni kuzamisha. Ukurasa 202**

Encyclopedia ya World Book	**Kanisa la kwanza lilitenda ubatizo kwa kuzamisha ndani ya maji. Toleo la 2, Uk.70**
Encyclopedia ya Kanisa la Kilutheri	**Martin Luther alitenda kuzamisha kama ukweli kuwa ukweli zaidi kuwa ni tendo la awali (toleo la 1, Ukurasa 188)**
Pulpit Commentary fasiri ya madhabahu iliyotolewa na wanazuoni waandishi	**Warumi 6:4 "Kuzikwa katika Ubatizo" Marejeo ni kubatiza kwa kuzamisha, (Toleo la 18, Ukurasa wa 156**

^^^

Biblia Inazungumza

Mathayo 28:19 **"Na kufundisha mataifa yote, "kufundisha au kuhubiri lazima kutanguliza ubatizo. Angalia Matendo 2:41.**

Matendo 8:36, 37 **Mkushi. "Ni nini kinanizuia nisibatizwe?" Filipo, "Kama ukiamini kwa moyo wako" Kuamini hutangulia ubatizo. Tazama Marko 16:16**

Matendo 2:38 **Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu" Toba lazima iandamane na ubatizo. Tazama Luka 24:47**

==========

Unajua……

Awali waliopokea ubatizo walikuwa ni watu wazima. Ubatizo wa watoto wachanga ni maendeleo yaliyoendea kunyunyizia.
(ENCYCLOPEDIA YA CHAMBERS, Toleo la 2, ukurasa wa 112)

Hakuna ushahidi wa wazi wa ubatizo wa watoto wachanga katika Agano Jipya. (INTERPRETERS BIBLE DICTIONARY, Toleo la 1, uk. wa 352)

Maandiko ya kale ya Kikristo haya zungumzi au kuandika ubatizo wa watoto wachanga. (ENCYCLOPEDIA BRITANNICA, Toleo 3, uk.138)

"……Ubatizo wa watoto wachanga awali ulitajwa mwaka wa 185BK, Haukujulikana katika dunia nzima hadi karne ya 6.
(HISTORIA YA KANISA, Iliyoandikwa na Walker, kurasa wa 87, 88)

Kwamba wachungaji 350 wa Kilutheri wa Ujerumani Magharibi walitaka kujitoa katika suala la ubatizo wa watoto, wengi wa hao wachungaji walikataa kuwabatiza watoto (vichanga) wao wenyewe. Walijisikia kwamba ubatizo unatakiwa ueleweke kwanza na wanaupokea.
TIME MAGAZINE, ukurasa wa 58, la Mei 1968)

Kwamba Karl Barth wa Swizaland mwana theologia anayejulikana katika karne ya 20 alisema "Hakuna msingi wa ki-Biblia kwa ajili ya ubatizo wa watoto – mapokeo haya ni mafundisho ya kale ya kosa la kanisa.
(TIME MAGAZINE, ukurasa wa 58, la Mei 1968)

Mtoto anatakiwa awe ana umri wa kutosha kupokea mafundisho , kuamini, na kutubu dhambi kabla ya kubatizwa.
Kuwaweka watoto wakfu kwa Mungu na kumwomba Awabariki ni Ki-Biblia.
Yesu alitenda katika Luka 18:15-17, Mathayo 19:13-15

-4-

UBATIZO

Je, uko katika Mpango wa Wokovu?

Yaliyoorodheshwa hapa chini (3) matatu ni kati ya sababu nyingi kwa nini ubatizo ni wa lazima kabisa.

BIBLIA INASEMA HIVYO!

"Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu." Commentary nyingi za Biblia zinakubali kwamba maji hapa inaelezea ubatizo. (Yohana 3:5).
(Angalia, Mathew-Henry, Adam Clark, History of Christian Church, Walker, Encyclopedia ya Catholic, Kamusi ya Oxford ya Kanisa, Interpreters Dictionary of the Bible, Temples Bible Dictionary.)

"Aaminiye na kubatizwa ataokoka" (Marko 16:16).
Tazama jinsi Yesu alivyounganisha ubatizo na wokovu.

"Ni sawa na ubatizo unaotuokoa sisi" (1 Petro 3:21) (*Pia tazama Matendo 10:6 na 48 Matendo 10:48 na Matendo 11:14.)*

UNAONDOA DHAMBI

Matumizi ya damu ya Yesu ni lazima katika kuondoa dhambi. Sasa basi ni kwa jinsi gani kupokea ondoleo la dhambi ki-Biblia. Jibu la swali hili litakuwa tu njia ya kupata damu ya Mwokozi kutumiwa. (Waebrania 9:22).

"Toba na ondoleo la dhambi vitahubiriwa katika Jina Lake" (Yesu) Luka 24:47.

"Tubuni Mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi…." Damu ya Yesu hutumika kupitia ubatizo wa maji katika jina la Yesu (Matendo 2:38). (*Pia tazama Yohana 5:8, na Matendo 22:16.*)

KUBATIZWA KATIKA KANISA

Kanisa lote la Agano Jipya lilifanywa na hao waliokuwa wamebatizwa katika imani baada ya kuamini na kubatizwa.
(Wagalatia 3:27 na 1 Wakorintho 12:13).

Kanisa katika Yerusalemu
3000 waliongezeka baada ya kuliamini neno (Matendo 2:41)

-5-

Kanisa katika Samaria
Wanaume na wanawake waliamini na kubatizwa. (Matendo 8:12-16)

Kanisa katika Kaisaria
Petro aliwaamuru wabatizwe katika jina la Yesu. (Matendo 10:48)

Kanisa katika Filipi
Lidia na bwana Jela wa Filipi walibatizwa (Matendo 16:14-33)

Kanisa katika Korintho
Paulo alihubiri. Waliamini na wakabatizwa (Matendo 18:8)

Kanisa katika Efeso
Paulo aliwabatiza tena wale waliokuwa wamebatizwa visivyo (Matendo 19:1-6)

Kanisa katika Galatia
Walimwamini Paulo. Na wakabatizwa katika Kristo. (Wagalatia 3:27)

Kanisa katika Kolosai
Walizikwa pamoja na Kristo katika ubatizo. (Wakolosai 2:12)

Kanisa katika Rumi
Waliifia dhambi, na kuzikwa kwa njia ya ubatizo (Warumi 6:1-4)

UBATIZO
Katika jina la…….

Baba, Mwana au Yesu Kristo?
na Roho Mtakatifu

Ni yapi katika haya yaliyotendwa na Mitume wa Kanisa la Kwanza?

Hapa chini ni mihimili miwili ya Maandiko yaliyoorodheshwa mahali Mitume aidha walifundisha au walitenda ubatizo wa maji.

Katika Jina la Yesu	**Baba Mwana, Roho na Roho Mtakatifu**

WAYAHUDI
"Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo"
(Matendo 2:38)

WASAMARIA
"Walikuwa wamebatizwa tu kwa jina la Bwana Yesu" (Matendo 8:16)

Katika Jina la Yesu	Baba Mwana, Roho na Rojo Mtakatifu

MATAIFA
"Akaamuru wabatizwe kwa jina la Bwana Yesu (Matendo 10:48)

PAULO ALIFUNDISHA
"Lolote mfanyalo kwa neno au kwa tendo fanyeni yote kwa jina la Bwana Yesu" Wakolosai 3:17)

PAULO ALIBATIZA
Paulo aliwabatiza tena kwa sababu walikuwa hawajabatizwa katika jina la Yesu. (Matendo 19:1-6)

Mathayo 28:19 yalikuwa ni maagizo yaliyotolewa na Yesu kubatiza katika Jina. Mitume hawakurudia maneno ya agizo, bali waliyatii kama inavyoonekana kwenye maandiko hapo juu. Kwa vile Baba Mwana na Roho Mtakatifu hivyo ni vyeo vya madhihirisho ya Roho Yenye nguvu na mwili Wake, Mitume walielewa jina Lake liokoalo ni Yesu.

Yuko yeyote atakayethubutu kusema kwamba Mitume hawakumtii Bwana, au walishindwa kubatiza ipasavyo?

JINA LA BABA, MWANA, NA ROHO MTAKATIFU
NI BWANA YESU KRISTO
Vitendo vya Mitume katika kitabu cha Matendo ya Mitume inathibitisha hili kuwa ni kweli.

Ubatizo katika jina la
BWANA YESU KRISTO

Ni jinsi gani Kanisa la kwanza lilivyotafsiri agizo la Kristo katika Mathayo 28:19?
Matendo ya Mitume 2:38, 8:16, 10:48 na 19:5 ni kumbukumbu nne za Ki-Biblia zinazojibu maswali haya. Kama kumbukumbu za Biblia hazitoshi, tafadhali jaribu kutafuta kumbukumbu za wasomi, waandishi na wana historia:

<u>Encyclopedia ya Britannica,</u> (Chapa ya 11, toleo la 3, ukurasa wa 365)
Ubatizo ulibadilishwa kutoka maneno katika jina la Yesu na kuwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu katika Karne ya 2.

<u>Encyclopedia ya Canney ya Dini,</u> (ukurasa wa 53)
Kanisa la kwanza lilibatiza kwa jina la Bwana Yesu hadi karne ya 2.

<u>Encyclopedia ya Hastings ya Dini,</u> (Toleo la 2)
***Ubatizo wa Kikristo ulitendwa kwa kutumia maneno, "Katika jina la Yesu* (ukurasa wa 377)**
***Ubatizo mara zote ulikuwa kwa jina la Yesu hadi wakati wa Justine Martyr (Mfia dini)* (ukurasa wa 389)**

<u>Ecyclopedia ya Katholiki</u>, (Toleo la 2 ukurasa 362)
Hapa mwandishi anakiri kwamba mfumo wa ubatizo ulikuwa umebadilishwa na kanisa lao.

<u>Encyclopedia ya kidini ya Schaf-Herzog,</u> (Toleo la 1 ukurasa 435)
Agano Jipya linajua tu ubatizo kwa jina la Yesu.

<u>Kamusi ya Biblia ya Hastings</u> (ukurasa wa 88)
Lazima kukiri kwamba majina ya pamoja ya Mathayo 28:19 hayaonekani kutumika na kanisa la kwanza, bali zaidi katika jina la Yesu, Yesu Kristo au Bwana Yesu.

Je! ni lazima kabisa jina la Yesu kutamkwa au kuitwa juu ya mtu wakati anapobatizwa?

Kwa jibu la swali hili tafadhali soma Matendo 15:17 na Yakobo 2:7 (wajihi wa Kigiriki) Wakristo wa Karne ya kwanza waliomba kwa au walililiitia jina la Yesu juu ya waamini katika ubatizo wa maji.

Kama baadhi wanavyosema, "Jina la Yesu ni kumaanisha mamlaka ya Yesu, basi zaidi sana *Jina,* kuliko vyeo, kuitiwa kwa anayebatizwa. Soma Mathayo 28:18, Matendo 4:12 na Wakolosai 2:9.

Yuda ni maonyo ya.. *"kuishindania imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu".(Tazama Wagalatia 1;8-9.)*

Je! Yuko yeyote anayethubutu kubadidilisha kile Kristo na Mitume walichokianzisha?

-8-